

**NYONGEZA NA. 1 YA MWONGOZO NA. 2 WA USIMAMIZI NA UDHIBITI
WA UBORA WA KOROSHO GHAFI KWA MWAKA 2023/2024**

S/N	MWONGOZO ULIVYOKUWA AWALI	NA.2 MABORESHO YA MWONGOZO NA.2 UTAKAVYOKUWA SASA
	SEHEMU YA NNE: UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI KATIKA GHALA LA MNADA Kipengele namba 4.5: Taratibu za Kutoa Korosho Ghala la mnada kipengele kidogo cha 4.5.4	
	Iwapo kutatokea tofauti ya daraja la ubora wa korosho, unyevu wa korosho na idadi ya korosho kwa kilo mnunuzi alizonunua mnadani mwendesha ghala atawajibika kuboresha na kuhakikisha mnunuzi anapata kiwango cha ubora na uzito alionunua au kumlipa mnunuzi utofauti wa bei kwa kuzingatia ubora. Aidha itakapothibitika tu ubora umeshuka Mwendesha ghala atawajibika kulipa Bodi ya korosho adhabu ya shillingi milioni moja (1,000,000/=) kwa kila kosa la ubora.	Iwapo kutatokea tofauti ya daraja la ubora wa korosho (SHOT), unyevu wa korosho (Moisture) na idadi ya korosho kwa kilo (Nut count) kwa korosho zilizohifadhiwa katika ghala la mnada wakati wa ukagazi utakaofanywa na Bodi ya korosho au kutakapokuwa na barua ya malalamiko ya ubora kutoka kwa mnunuzi aliyenunua korosho hizo. Mwendesha ghala atawajibika kuboresha na kuhakikisha mnunuzi anapata kiwango cha ubora na uzito alizonunua au kumlipa mnunuzi utofauti wa bei kwa kuzingatia ubora. Aidha itakapothibitika ubora wa korosho zilizohifadhiwa ghalani umeshuka au taratibu zilizoelekezwa kwenye Mwongozo huu hazijafuatwa, Mwendesha ghala atawajibika kulipa Bodi ya korosho faini ya shillingi milioni moja (1,000,000/=) kwa kila kosa la ubora litakalothibitika.
	SEHEMU YA TANO: MAJUKUMU NA WAJIBU WA WADAU KATIKA KUSIMAMIA UBORA WA KOROSHO GHAFI Kifungu cha 5.3: Majukumu ya Mwendesha ghala katika kudhibiti ubora wa korosho ghafi kifungu kidogo cha 5.3.1	

	Mwendesha ghala anapaswa kuwa na vifaa vya ubora kama vilivyoainishwa katika kipengele 4.3 na viwe vimehakikiwa na mamlaka husika (TBS na WMA). Vifaa vyote viwepo ghala la mnada kabla ya zoezi la kupokea Korosho kuanza. Iwapo mwendesha ghala atathibitika kuwa na vifaa pungufu au havijahakikiwa na mamlaka husika. Mwendesha ghala atawajibika kulipa Bodi ya Korosho faini ya shilingi laki tano (500,000/=).	Mwendesha ghala anapaswa kuwa na vifaa vya ubora kama vilivyoainishwa katika kipengele 4.3 na viwe vimehakikiwa na mamlaka husika (TBS na WMA). Vifaa vyote viwepo ghala la mnada kabla ya zoezi la kupokea Korosho kuanza. Iwapo mwendesha ghala atathibitika kuwa na vifaa pungufu au havijahakikiwa na mamlaka husika. Mwendesha ghala atawajibika kulipa Bodi ya Korosho faini ya shilingi laki tano (500,000/=).
--	---	---

KWAMBA, vifungu vya Mwongozo Na.1 ambavyo havijafanyiwa marekebisho na Nyongeza hii vitaendelea kusomeka na kutekelezwa kama vilivyo.

Nyongeza hii imetolewa na kusainiwa leo tarehe 22 Novemba, 2023.



Francis Alfred

MKURUGENZI MKUU